

Ukiushi wa Taswira Dumifu za Uana katika Ugavi wa Kazi na Majukumu: Tathmini ya Hadithi Teule za Kiswahili za Watoto

Simon Ekiru¹, Mosol Kandagor² na Magdaline Wafula²

¹Chuo Kikuu cha Turkana

²Chuo Kikuu cha Moi

Ikisiri

Makala hii inachunguza ukiushi wa taswira dumifu za uana katika ugavi wa kazi na majukumu kwenye hadithi za Kiswahili za watoto. Lengo kuu hasa ni kupambanua namna ambavyo ugavi wa kazi na majukumu kwenye hadithi teule za Kiswahili za watoto umekiuka taswira dumifu za uana. Nadharia ya Udenguzi ilitumika kuwa kiunzi cha nadharia na vilevile katika uchanganuzi wa data. Utafiti huu ulizingatia muundo wa kimaelezo na mbinu ya uhakiki makinifu wa matini. Data iliyotumika katika makala hii ilitokana na uhakiki wa hadithi 11 za Kiswahili za watoto. Hadithi zilizochanganuliwa zilisampulishwa kimakusudi kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti ulifanywa kwa kutumia maelezo. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa kazi kama vile ualimu, udaktari, uaskari, uanajeshi, urubani, ukulima, uhadhiri, ufanyi biashara, na uhakimu ulifanywa na wahusika wa kike. Aidha, majukumu kama vile kulima, kufyeka, kusukuma toroli, kulisha ng'ombe, na kuchunga mifugo yalifanywa na wahusika wa kike huku wahusika wa kiume wakitekeleza majukumu kama vile kuosha vyombo na kuandika meza. Kwa kuhitimisha, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa taswira dumifu za uana zimekiukwa katika ugavi wa kazi na majukumu, kwenye hadithi za Kiswahili za watoto. Makala hii hivyo basi inapendekeza matibaa, mashirika ya kuchapisha vitabu vya watoto na asasi za kiserikali zibuni sera na miongozo itakayohakikisha kuwa taswira dumifu za uana zinadhibitiwa hususan katika ugavi wa kazi na majukumu. Mwisho, makala hii pia imedhihirisha kuwa fasihi ya Kiswahili ya watoto ni nyenzo muhimu katika Jitihada za utatuzi wa migogoro ya kiuana ambayo huathiri mahusiano ya kijinsia katika jamii.

Maneno Muhimu: *Taswira Dumifu, Uana (TDU), Kazi, Majukumu*

Utangulizi

Makala hii inapambanua ukiushi wa taswira dumifu za uana katika ugavi wa kazi na majukumu kwa wahusika wa kiume na wa kike kwenye hadithi teule za Kiswahili za watoto. Upambanuzi umefanywa kwa kutambua na kuchambua kazi na majukumu mbalimbali ambayo wahusika kwenye hadithi teule za Kiswahili za watoto wametengewa. Makala hii inaanza kwa kutoa mjadala mfupi kuhusu usawa wa uana na jinsia. Aidha, imetoa ufafanuzi kuhusu dhana ya taswira dumifu za uana. Baada ya hapo, imebainisha msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya na kuchanganua data. Hatimaye matokeo ya utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo yamewasilishwa.

Usawa wa Uana na Jinsia

Tangia kuzuka kwa mijalada ya kiusomi na utafiti kuhusu masuala ya uana na jinsia Kusini mwa Jangwa la Sahara, hatua kubwa imepigwa kuhusu uhamasishaji wa usawa wa uana (Onyango, 2007). Baadhi ya mambo ambayo yameshughulikiwa ni kama vile: dhuluma za uana zinazowaathiri wanawake, elimu duni kwa wanawake na ukandamizwaji wa wanawake katika nafasi za ajira na uongozi. Ijapokuwa hatua hizi zimepongezwa na mashirika ya kutetea haki za kibinadamu kama vile Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia utamaduni na elimu (UNICEF), Onyango (2006) anahoji kuwa, jitihada hizi zimekuwa zikiegemea jinsia ya kike na kupuuza jinsia ya kiume.

Hali hii imewafanya wasomi wakiwemo Miricho na Mbuthia (2017) kudai kuwa kuna uwezekano wa kuzuka tena kwa migogoro ya kijinsia baina ya jinsia ya kiume na ya kike, kwa sababu wanaume huhisi kuwa wametelekezwa na kukandamizwa katika jamii. Ili kuzuia migogoro kama hii, mbinu

nyinginezo za kimakusudi zilianzishwa kupitia miradi ya kuchapisha vitabu vinavyosawiri uana kwa mitazamo inayokiuka taswira dumifu za uana ambazo zilikuwa zimekithiri hapo awali (Nhundu, 2007; Miller, 2013).

Kwa kutambua umuhimu wa usawa wa uana, matibaa yalianza kuchapisha vitabu vinavyosawiri wahusika wa kike na wa kiume kwa mtazamo sawa. Matibaa ya Macmillan ndiyo iliyokuwa ya kwanza kuchapisha vitabu vya kiada vilivyozingatia usawa wa uana. Kwa mujibu wa Briton na Humpkin (1997), falsafa iliyoandisi matibaa ya Macmillan ni kuwa; *“Dhima ya vitabu si kuwawezesha tu watoto kuboresha uwezo wao wa kusoma au kukokotoa hisabati; vitabu vina jukumu la kuwaelimisha wabaini namna jamii inavyofasiri makundi mbalimbali ya watu hususan katika misingi ya uana”* Maoni yao yanawiana na yale ya Ginn na wenzake (1973) walioamini vifaa vya kufundishia vilifaa kuwasaidia wanafunzi kujenga mitazamo chanya kuhusu maisha yao, dini yao, nchi yao, jamii yao, uana wao miongoni mwa mambo mengine muhimu ya kimsingi yaliyowaathiri.

Fox (1993) anadai kuwa vitabu vina uwezo wa kuathiri jinsi binadamu anavyojifahamu na kujitambualisha katika misingi ya uana. Vitabu hasa vile vya watoto vinapowasilisha taswira dumifu za uana katika hadhira yake ambayo aghalabu huwa ni watoto, kuna uwezekano wa watoto kufumbata taswira hizo dumifu za uana (Matundura, 2007; Onyango, 2007; Floyd, 2012; Mbuthia 2018).

Athari ya taswira hizi dumifu za uana ni kuwa, watoto huishia kujenga imani kuwa jinsia fulani ni dhalili na dhaifu inapoliganishwa na nyingine (Morrow, 2006; Ezenwa-Ohaeto, 2015; Miricho na Mbuthia, 2017). Taasubi hizi za uana zinaweza kukolea na kukomaa akilini mwao toka utotoni hadi ukubwani (Golshirizian, Dhillon, Maltz, Payne na Rabow, 2015). Hali hii inaweza kusababisha kuwapo kwa kizazi kinachobaguana katika misingi ya uana (Floyd, 2012).

Ni kutokana na haya ndipo baadhi ya mataifa duniani kama vile Norway na Zimbabwe yalibuni sera na miongozo iliyohimiza uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya watoto vinavyoendeleza taswira huria za uana. Norway ilianzisha mradi wa kuchapisha vitabu vilivyoeendeleza usawa wa uana katika shule za chekechea uliojulikana kama *“Action Plan for Gender Equity”* (2008). Zimbabwe vile vile kama anavyodai Nhundu (2007) ilianzisha mradi uliojulikana kama Gender Equity Literature (GEL) kukabili taswira dumifu za uana katika shule za msingi. Mradi huo ulilenga kutumia hadithi za watoto wa kike kuvunja taasubi hasi za uana na kujenga imani kuwa wanawake pia wanaweza kufanya kazi au majukumu yanayofanywa na wanaume.

Mbinu hii ya kutumia vitabu vilivyokiuka taswira dumifu za uana inapendekezwa na wasomi kama vile, Miller (2013) pamoja na Derma Sparks na Edward (2010). Hali hii imechochea mabadiliko katika utunzi wa vitabu vya hadithi vya watoto ambavyo vimejaribu kukiuka taswira dumifu za uana. Ni kutokana na mjadala huu, ndipo utafiti huu ulizuumu kubainisha iwapo fasihi ya Kiswahili ya watoto imefuata mkumbo wa kiulimwengu na kukiuka taswira dumifu za uana.

Dhana ya Taswira Dumifu za Uana (TDU)

Taswira dumifu za uana ni mwelekeo wa kimawazo ambao huchupizwa akilini mwa watoto wadogo ili wanapokua, waamini kuwa yapo mambo tofauti yanayohusishwa na wanaume pamoja na wanawake (Liben na Signorella, 1980; Preece na Bullingham, 2022). Kwa namna nyingine, haya ni majukumu, sifa na itikadi zinazoaminika kuwa ni za wavulana au wasichana pekee. Meland (2020) anadai kuwa taswira dumifu ni mitazamo ya kiitikadi au kiakili aliyonayo mtu kumhusu mtu mwingine wa jinsia fulani. Mitazamo hiyo inaweza kuwa chanya au hasi kuwa sifa bainifu na za kijumla kuhusu kundi husika la watu katika jamii.

Msomi wa saikolojia ya jamii aliyejulikana kama Biem ndiye anayetambulika kwa juhudi zake za kupambanua mchakato wa jamii unaoeneza taswira dumifu za uana (Martin na Halverson, 1981; Biem, 1981, 1983). Biem (1993) katika nadharia yake ya muundo wa uana (Gender- Schemata theory) au Nadharia ya Biem (Biem's Theory), anadai kuwa jamii huunda itikadi, dhana, au taswira mbalimbali za kijamii. Taswira hizi huhusishwa na watu wa jinsia fulani katika jamii husika.

Mtoto anapozaliwa na kukuzwa katika mazingira ya jamii maalum hupokezwa maarifa au habari kuhusu muundo wa uana katika jamii. Mtoto huelekezwa kufahamu habari, imani, mitazamo, sifa, majukumu, itikadi na mambo mengine yayohusishwa na wanawake au wanaume katika jamii yake. Kwa hivyo mtoto huyu hukua akifahamu mwanamke na mwanamume ni watu tofauti wenye dhima na

uwezo tofauti katika jamii. Taswira hizi zinapokolea na kukomaa akilini mwa mtoto huyo, huunda taswira kolevu na komavu zinazojulikana kama taswira dumifu. Taswira hizi zinapohusishwa na watu wa jinsia husika hujulikana kama taswira dumifu za uana.

Kimsingi, taswira dumifu za uana (TDU) ni nadharia wanazopandikiziwa watoto au watu katika jamii fulani kuhusu sifa za wanaume au wanawake katika jamii husika. Ni mawazo, itakadi, imani, majukumu, hadhi na kadhalika zinazohusishwa na wanaume au wanawake katika jamii husika.

Msingi wa Kinadharia

Nadharia ya Udenguzi ndiyo iliyotumika kuchunguza ukiushi wa taswira dumifu za uana katika ugavi wa kazi na majukumu kwenye hadithi teule za Kiswahili za watoto. Mwasisisi wa Nadharia ya Udenguzi ni mwanafalsafa wa Kifaransa Jacques Derrida katika kazi yake *De la Grammatologie (Of Grammatology)* ambapo aliangazia suala la lugha na maana (Derrida, 1976). Nadharia ya udenguzi huonyesha kuwa ni vigumu kwa matini kuwa na maana moja maalumu na isiyobadilika (Miricho, 2021). Kwa hivyo Derrida, alihimiza jukumu la msomaji kubainisha maana nyinginezo. Hata hivyo, makala hii ilijikita tu katika mhimili mmoja wa udengeuzi. Mhimili huu ni udenguzi kuwa ukiushi wa kaida za matini. Mhimili huu ulitumika kuonyesha namna waandishi wa hadithi za Kiswahili za watoto walivyokiuka kaida za uandishi ambazo zimekuwa zikiegemea ugavi wa kazi na majukumu kwenye hadithi za watoto. Kaida hizi zimekuwa zikiegemeza ugavi wa kazi na majukumu kufanywa katika misingi ya taswira dumifu za uana.

Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kutumia muundo wa maelezo na mbinu ya uhakiki makinifu wa matini teule. Hadithi za Kiswahili za watoto zilizohakikiwa ndizo zilizokuwa msingi wa data katika makala hii. Hadithi hizi ziliteuliwa kimakusudi ili kukidhi madhumuni ya utafiti. Utafiti ulilenga kupambanua namna ukiushi wa taswira dumifu za uana katika ugavi wa kazi na majukumu unavyojitokeza kwenye hadithi za Kiswahili za watoto. Nadharia ya Udenguzi ilitumika kuwa kiunzi cha kinadharia na vilevile katika uchanganuzi wa data husika. Data iliyochanganuliwa ilitokana na maelezo kutoka kwa matini pamoja na vielelezo kwenye hadithi teule. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kurejelea hadithi teule za Kiswahili za watoto ambazo ni: *Sungura Mjanja* (Islam, 2008), *Tuzo ya Baba* (Zawadi, 2013), *Atoke Asitoke* (Mwangi, 2010), *Siku za Juma* (Nyakeri, 2006), *Kombo Arudi Shule* (Lewela, 2008), *Vitendo vya Jamila* (Mogambi, 2008), *Rangi Zetu* (Agume, 2015), *Khadija na Baiskeli Nyekundu* (Kalindimya, 2008), *Kiki Afunga Bao* (Rukaria, 2008), *Kisa cha Mebo* (Atuto, 2008), na *Furaha ya Arope* (Walibora, 2013).

Matokeo ya Utafiti

Kazi na Majukumu katika Hadithi Teule za Watoto

Dhana ya kazi katika muktadha wa utafiti huu inarejelea nafasi au ngazi mbalimbali za ajira katika jamii kama vile: Udaktari, ualimu, uanajeshi, useremala, uwakili, uhakimu na kadhalika. Dhana ya majukumu inarejelea wajibu au shughuli mbalimbali ambazo wahusika katika hadithi teule za watoto wameshirikishwa kwazo. Majukumu katika utafiti huu ni kama vile: Kufua, kupika, kufyeka, kulima, kuongoza watu wengine michezoni, kushiriki michezoni, kushiriki katika shughuli za shuleni na nyumbani na kadhalika. Kwenye hadithi teule zilizotumika katika utafiti huu, wahusika walishirikishwa katika kazi na majukumu mbalimbali. Wapo wahusika waliosawiriwa kuwa madaktari, walimu, askari, rubani, waandishi, wataalamu wa kuchimbua mafuta, na hakimu. Wahusika wengine walisawiriwa kushiriki katika majukumu ya nyumbani kama vile kupika, kuosha vyombo, kufyeka, kunadhifisha mazingira, kubeba mchanga au uchafu kwa toroli, kuchunga mifugo miongoni mwa mengine. Aidha, wahusika wengine walishirikishwa kucheza michezo kama vile soka, kuruka kamba, kupanda miti miongoni mwa mengine.

Tulibainisha kazi na majukumu mbalimbali walivyotwikwa wahusika kwa njia mbili. Kwanza, tulitumia maelezo yaliyotolewa kuwahusu au kuhusu mambo waliyojishughulisha nayo katika hadithi teule. Pili, tulichanganua vielelezo vilivyowasilishwa katika hadithi husika. Ili kutambua aina ya kazi au majukumu ambayo mhusika fulani katika kielelezo alikuwa ametengewa, tulitumia tajriba na umaizi wetu kuhusu mitindo ya mavazi na vifaa mbalimbali vinavyohusishwa na kazi fulani katika

jamii nyingi ulimwenguni. Kwa mfano, tuliweza kutambua picha ya mhusika fulani kuwa ni askari (polisi au jeshi) na hasa nchini Kenya alipoonekana kavaa magwanda ya askari huku amebeba bunduki mkononi.

Ukiushi wa Taswira Dumifu za Uana katika Ugavi wa Kazi

Kwa mujibu wa vielelezo na maelezo yaliyowasilishwa, ni bayana kuwa wahusika wa kike na wa kiume walitwikwa kazi mbalimbali katika hadithi teule. Wahusika wa kike aghalabu walisawiriwa kufanya kazi kama vile: Ualimu, udaktari, uhakimu, uhadhiri, upolisi, ufanyi biashara, na ukulima. Vilevile, yupo mhusika wa kike aliyeitwa Arope aliyewazia kufanya kazi kama vile rubani, daktari, mwanajeshi, polisi, mwalimu au mwandishi, pindi atakapomaliza masomo (Taz. Furaha ya Arope, Uk.7). Wahusika wa kike waliosawiriwa kuwa walimu ni kama vile: Mwalimu aliyevaa skafu nyekundu katika hadithi ya *Sungura Mjanja* (Taz. Uk.4 na 5), Mwalimu Anyanga katika hadithi ya *Upinde wa Mvua* (Taz. Uk.10), Mwalimu Atieno katika hadithi ya *Kiki Afunga Bao* (Taz. Uk.10 na 11), Bi. Chebii katika hadithi ya *Khadija na Baiskeli Nyekundu* (Taz. Uk.19) na Mwalimu wa Arope katika hadithi ya *Furaha ya Arope* (Taz. Uk.8). Aidha tunamwona Arope katika hadithi ya Furaha ya Arope akisema kuwa, angependa kuwa rubani, daktari, mwanajeshi, polisi, mwalimu au mwandishi. Arope anasema hivi:

“Mimi najaribu kuwa mwerevu na mwenye tabia nzuri. Ninataka kusoma niwe daktari au mwalimu, au rubani. Ninataka pia kuwa mwanajeshi, au mwandishi, au mtaalamu wa kuchimbua mafuta...”
(Taz. Uk.6)

Wahusika wa kiume waliohusishwa na kazi ya ualimu ni kama vile: Mwalimu mkuu katika hadithi ya *Sungura Mjanja* (Taz. Uk.4 na 5), na Mwalimu wa Kombo katika hadithi ya *Kombo Arudi Shule* (Taz. Uk.14). Kwa ujumla, wahusika 6 wa kike waliohusishwa na kazi ya ualimu huku wahusika 2 pekee wa kiume ndio waliohusishwa na kazi hiyo.

Kazi nyingine iliyoangaziwa katika hadithi teule ni udaktari. Katika hadithi zote zilizohakikiwa kwenye utafiti huu, ni wahusika wa kike pekee ndio walionasibishwa na udaktari. Kwa mfano, katika hadithi ya *Furaha ya Arope* tunamwona Arope akitazamia kuwa daktari pindi atakapomaliza masomo (Taz. Uk.6). Mfano mwingine ni mhusika Mebo kwenye hadithi, *Kisa cha Mebo*, aliyesoma kwa bidii na kuwa daktari (Taz. Uk.11 na 14).

Kazi ya upolisi, ukulima, useremala, kinyozi, uchifu, ufanyi biashara, udereva na uhakimu pia zimeangaziwa katika hadithi teule zilizotumika katika utafiti huu. Kwa mfano, katika hadithi ya *Sungura Mjanja*, tunaieleza kuwa Sungura alipopita kijijini, alimwona mkulima na seremala. Alimwona kinyozi na mchungaji. Alimwona askari (polisi) na chifu. Vielelezo vilivyowasilishwa (Taz. Uk. 8 na 9) vilionyesha kuwa mkulima na askari (polisi) walikuwa wa jinsia ya kike huku seremala, kinyozi, chifu na mchungaji wakiwa wa jinsia ya kiume. Aidha, hadithi iyo hiyo (Taz. Uk.6 na 7) iliwasawiri wauzaji au wafanyabiashara sokoni kuwa wa jinsia zote mbili, kwa kuwasilisha wahusika wa kike na wa kiume wakichuza vyakula mbalimbali sokoni. Katika hadithi ya *Kisa cha Mebo*, tunamwona hakimu wa jinsia ya kike akiwahukumu Bwana na Bibi Mateso kortini kwa kosa la kumtesa Mebo (Taz. Uk.14). Aidha, tunamwona mhadhiri wa kike, ambaye pia ni naibu chansela wa chuo akimkabidhi Mebo cheti cha kufuzu shahada ya udaktari (Taz. Uk.11). Mwisho, katika hadithi ya *Khadija na Baiskeli Nyekundu*, tunamwona mama ya Khadija akimpeleka kila siku shuleni kwa gari. Msimulizi anatueleza hivi:

“Khadija alikuwa mwanafunzi mtiifu shuleni. Kila siku asubuhi mamake alimpeleka shuleni kwa gari...” (Taz. Uk. 1)

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa ugavi wa kazi katika hadithi teule ulikiuka TDU. Hii inatokana na misingi kuwa, baadhi ya kazi ambazo waandishi wa hadithi hizi waliwapa wahusika wa kike zinaaminika kuwa kazi zinazopaswa kufanywa na wanaume katika jamii nyingi ulimwenguni (Mizra, 2004; Ullah, 2013). Mifano ya kazi hizi ni kama vile: ualimu, udaktari, uaskari/upolisi, uanajeshi, urubani, ukulima, uhadhiri, unaibu chansela wa chuo, ufanyibiashara, na uhakimu. Hali hii ya kugawa kazi katika misingi ya uana inasababishwa na mfumo wa jamii ambao hubagua hunasibisha baadhi ya kazi na jinsia fulani. Katika mchakato wa ugavi wa kazi, mfumo huu mara

nyingi hupendelea mfumo wa kuumeni na kutelekeza mfumo wa kuukeni hususan katika ugavi wa kazi zinazoaminika kuwa za hadhi ya juu kisiasa, kiuchumi na kijamii (Ezenwa-Ohaeto, 2015). Wanaume katika jamii nyingi ulimwenguni wamesawiriwa kuwa binadamu wenye nguvu, ujuzi na uwezo wa kufanya kazi zinazohitaji nguvu, utaalumu na ubunifu wa kiwango cha juu huku wanawake wakisawiriwa kama wategemezi wao (Essen, 2007). Tafiti za awali zikiwemo (Mizra na Malik, 1999; Ellis, 2002; Mizra, 2004; Ullah, 2013) zilionesha kuwa wanawake walihusishwa na kazi za nyumbani huku wanaume wakihusishwa na kazi za kiuchumi au zinazoleta pesa.

Utafiti wa Ellis (2002), kwa mfano, ulionyesha kuwa katika vitabu vilivyotumika katika shule za taifa la Bengali Magharibi, hakuna hata mhusika mmoja wa kike aliyesawiriwa kufanya kazi ambayo ingemwezesha kuzumbua riziki ili kuisaidia familia na jamii yake. Wahusika wote wa kike walihusika na kazi zisizo na ujira wala malipo. Isitoshe, hakuna mhusika wa kike aliyehusishwa na kazi yoyote katika sekta ya umma.

Utafiti wa Essen (2007) vilevile ulionyesha kuwa, wahusika wa kiume ndio walioshirikishwa katika kazi zinazohitaji utaalumu. Wahusika wa kike walipewa majukumu ya nyumbani. Ni wahusika wachache tu wa kike ndio waliopewa kazi ya uuguzi na ualimu katika elimu ya msingi na chekechea. Kimmel (2004) pia katika utafiti wake uliojulikana kama *'The Gendered Society'* anadai kuwa wahusika wa kiume walipewa kazi za nje ya nyumba (Outdoors chores) huku wahusika wa kike wakipewa kazi za ndani ya nyumba (domestic chores).

Mizra na Malik (1999) wakitathmini kazi zilizohusishwa na wahusika katika vitabu vya watoto nchini Pakistan walibaini kuwa, wahusika wa kike walipewa kazi za nyumbani kama vile kupika huku wahusika wa kiume wakisawiriwa kama wapiganaji vitani, wafanyabiashara, nahodha, rubani, na madereva. Utafiti sawa na huo ni utafiti uliofanywa na Ullah (2013). Ullah (keshatajwa), aliorodhesha kazi zilizosawiriwa kuwa za wanaume na wanawake katika vitabu vya kiada nchini Pakistan. Wahusika wa kiume walisawiriwa kuwa wakulima, wafanyabiashara, wawindaji, madereva, fundi viatu, seremala, masonara, wavuvi, wanajeshi, polisi au askari, askari wa kulinda misitu, wasimazi au mameneja wa benki, manahodha, marubani, watumishi wa posta, mabazazi, wahadhiri wa vyuo vikuu na walimu. Wahusika wa kike walihusishwa na kazi kama vile: wauguzi, wahudumu wasaidizi wa benki, wahudumu wa kupokea simu (telephone operators), wasaidizi katika kampuni za magazeti na kazi za nyumbani kama ujakazi.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa ugavi wa kazi hususan miongoni mwa wahusika wa kike katika hadithi teule, ulikiuka TDU. Waandishi wa vitabu hivi waliwapa wahusika wa kike kazi zinazoaminika kuwa za wanaume. Wanawake walihusishwa na kazi za kifahari kama vile ualimu, udaktari, uhakimu, uhadhiri, uaskari, urubani, uanajeshi, na udereva ambazo kwa mujibu wa tafiti tulizorejelea, zilihusishwa na wanaume. Aidha, ugavi wa kazi kama vile ukulima kwa wahusika wa kike, umekiuka itikadi kuwa wanawake hawawezi kufanya kazi zinazohitahaji nguvu.

Wanawake katika hadithi hizi vilevile wamepewa kazi katika sekta mbalimbali za umma zinazowawezesha kuzumbua riziki na kujichumia hela zinazowawezesha kusaidia na kukimu familia na jamii zao. Mfano bora ni Mwalimu Chebii katika Hadithi ya *Khadija na Baiskeli Nyekundu* anayetumia hela alizozipata kutokana na kazi yake ya ualimu kumnunulia Khadija zawadi ya baiskeli nyekundu (Taz. Uk.19).

Matokeo haya yamedhihirisha nguvu na uwezo wa waandishi katika ubomozi na uumbaji upya wa jamii kupitia fasihi (Derrida, 1976). Muundo wa uana uliozoeleka katika jamii nyingi umedenguliwa na kusawiriwa upya katika hadithi hizi. Ni wazi kuwa, waandishi wa hadithi za watoto wamezuumu kukiuka kaida zilizozoeleka katika usawiri wa wahusika ili kukweza hadhi ya wahusika wa kike. Wamefanya hivi kwa kuwakweza wahusika wa kike ambao walikuwa wametwezewa katika hadithi za awali. Yamkini, wamefanya hivi kimaksudi ili kutoa ujumbe kwa umma kuwa ulimwengu wa sasa umebadilika hivyo jamii za Kiafrika ambazo ndizo muktadha pokezi wa hadithi hizi hazina budi kubadilisha ufasiri wao katika miundo ya uana. Akishadidia wazo hili, Rorty (1996) anadai kuwa utokeaji wa ukiushi katika mkabala wa udenguzi si ajali bali hucusudia kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Maelezo haya ya Rorty yanatupa taswira halisi ya mabadiliko yanayoweza kutokea katika uundaji wa matini.

Kama ilivyobainika katika tafiti tangulizi (Matundura, 2007; Onyango, 2007), uandishi wa hadithi za Kiswahili za watoto hapo awali ulifuata mifumo ya jamii husika ambao ulizingatia muundo wa uana uliojengwa kwa mujibu wa utamaduni, dini, mila, na itikadi zilizozoeleka na kuaminika kuwa msingi wa jamii husika. Hata hivyo, utafiti huu umedhihirisha kuwa muundo wa uana unaweza kukiukwa katika uandishi wa kazi za kifasihi. Ukiushi huo umetokana na uundaji wa maana ya uana ambapo katika hadithi teule zilizohakikiwa, waandishi wamejaribu kufasiri upya maana ya uana kwa kuonyesha kuwa uana ni dhana nasibu isiyo na unasaba au athari yoyote katika ugavi wa kazi katika jamii. Aidha, waandishi hawa wamefasiri maana ya uana kwa namna tofauti ilivyofasiriwa na waandishi wa hadithi za awali.

Wafula na Njogu (2007) wanadai kuwa mojawapo ya sifa kuu ya udenguzi ni kumpa mhakiki au msomaji jicho pevu la kutazama na kuvumbua kile ambacho wahakiki au wasomaji wengine hawajakiona au hawajakifasiri. Udenguzi pia humpa mhakiki au msomaji uwezo kwa kufasiri maana tofauti na wahakiki na wasomaji wengine. Ni kwa misingi hii ndipo waandishi wa hadithi teule, ambao ni wahakiki na wasomaji wa miundo ya uana katika jamii, walichukua mwelekeo tofauti na wenzao wa awali na kuzuumu kufasiri upya na kwa namna tofauti miundo ya uana kupitia hadithi teule.

Ukiushi wa Taswira Dumifu za Uana katika Ugavi wa Majukumu

Kulingana na data iliyowasilishwa kutoka kwa vielelezo na maelezo katika hadithi teule, ilibainika kwamba, wahusika wa kike na wa kiume walihusishwa katika majukumu mbalimbali. Majukumu haya ni kama vile: Kufua, kupika, kufyeka, kulima, kuongoza watu wengine michezoni, kushiriki michezoni, kushiriki katika shughuli za shuleni na nyumbani.

Tafiti za awali kuhusu ugavi wa majukumu miongoni mwa jamii za Kiafrika (k.v. Mwaba, 1992; Mosley, 2004; Wanjeri, 2006), zilionesha kuwa wanaume na wanawake hupewa majukumu katika misingi ya uana. Jamii za Kiafrika zimetenga majukumu yanayopaswa kutekelezwa na wanawake na yale yanayopaswa kutekelezwa na wanaume. Kwa mfano, katika taifa la Afrika Kusini, Mwaba (1992) anadai kuwa wavulana na wasichana wengi katika shule za sekondari nchini Afrika Kusini waliamini kuwa kazi na majukumu kama vile uuguzi, kunadhifisha nyumba, kuosha vyombo, kufua, kufagia nyumba au boma na majukumu yote ya nyumbani yalipaswa kufanywa na wanawake huku wanaume wakipaswa kufanya majukumu yanayohitaji nguvu na maarifa mengi.

Mosley (2004) vilevile anadai kuwa, katika taifa la Uhabeshi, majukumu ya kunadhifisha nyumba, kuchota maji, kupika na kufua yaliaminika kuwa ya wanawake huku wanaume wakitarijiwa kujikita katika majukumu 'magumu' kama vile kulima, kufyeka, kusukuma au kubeba vifaa vizito n.k. Katika jamii ya Wakikuyu nchini Kenya, Wanjeri (2006) anadokeza kuwa, wavulana walielekezwa kufanya majukumu yaliyotajwa kuwa ya kiume kama vile: kuchunga mifugo, kuwinda, kujenga nyumba, kulima, kufyeka miongoni mwa mengine. Kwa upande mwingine, wasichana wa katika jamii ya Wakikuyu walifunzwa majukumu yaliyoaminika kuwa ya kike kama vile: kunadhifisha nyumba, kuosha vyombo, kupika, kuwatunza watoto miongoni mwa majukumu mengineyo waliyotarajiwa kufanya nyumbani.

Matokeo ya tafiti hizi (Mwaba, 1992; Mosley, 2004; Wanjeri, 2006) zinawiana na matokeo ya tafiti yakiwemo (k.v. Mizra na Malik, 1999; Kimmel, 2004; Ahmed, 2006; McCabe na wenzake, 2011; Ullah na Skelton, 2012), ambazo pia zilihusu usawiri wa majukumu ya wahusika katika vitabu vya kiada shuleni. Mizra na Malik (1999), kwa mfano, wanadai kuwa wahusika wa kike walipewa majukumu ya kupika, kufua nguo na majukumu mengine ya nyumbani huku wahusika wa kiume wakipewa majukumu kama vile kupigana vitani na shughuli nyinginezo zilizohitaji nguvu nyingi kutekelezwa.

Katika utafiti wa Kimmel (2004), wahusika wa kiume walipewa majukumu ya nje ya nyumba (Outdoors activities) huku wahusika wa kike wakijukumishwa hamkani za ndani ya nyumba (Indoors activities). Utafiti wa Ahmed (2006) pia unaonyesha kuwa licha ya serikali ya India kuisitiza kuondolewa kwa TDU katika vitabu vya watoto, waandishi bado waliendelea kuwajukumisha wahusika wa kike kutekeleza majukumu kama vile: Kuchota maji, kupika, kusafisha nyumba na kadhalika. Matokeo hayo ni sawa na yale ya McCabe na wenzake (2011) na Ullah na Skelton (2012),

ambayo yalionyesha kuwa vitabu vya watoto viliwasawiri wahusika wa kike wakishiriki katika majukumu kama vile: Kupika, kufanya usafi (cleaning), kufagia, kufua nguo, kuchota maji, kuwalea watoto, kuosha vyombo pamoja na kazi nyingine za nyumbani.

Katika muktadha wa fasihi ya watoto ya Kiswahili, utafiti wa Matundura (2007) ndio ulioshughulikia ugavi wa majukumu katika hadithi za Kiswahili za watoto. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa waandishi wa hadithi za Kiswahili za watoto waliwapa wahusika majukumu yaliyofumbata TDU. Wahusika wa kike walipewa majukumu ya ndani ya nyumba huku wahusika wa kiume wakipewa majukumu ya nje ya nyumba.

Hata hivyo, matokeo katika utafiti huu yanatofautiana na matokeo yaliyowasilishwa katika tafiti za awali. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa waandishi wa hadithi teule wamewapa wahusika wa kike majukumu yanayoaminika kuwa ya wanaume huku wanaume wakipewa majukumu yanayosadikiwa kuwa ya wanawake. Wahusika wa kike wameonekana kutekeleza majukumu ya nje ya nyumba huku baadhi ya wahusika wa kiume wakitekeleza majukumu ya ndani ya nyumba. Kwa mfano, katika hadithi ya *Siku za Juma* tunawaona wahusika wakuu wawili ambao ni Juma (mvulana) na Maria (msichana) wakifanya kazi ya kuwapa kuku mahindi (Taz. Uk.6). Jukumu la kulea kuku na wanyama wadogo wa nyumbani katika jamii nyingi za Kiafrika huaminika kuwa la wanawake. Wanaume hushiriki katika shughuli ya kuwalisha mifugo wakubwa kama vile: ng'ombe, mbuzi, ngamia, punda, farasi, nguruwe na kadhalika (Mosley, 2004). Katika hadithi ya *Siku za Juma* tunamwona Juma, ambaye ni mhusika wa kiume akihusishwa na jukumu la kuwapa kuku chakula, ambalo linaaminika kuwa shughuli ya wanawake au wasichana. Mwandishi wa hadithi hii (Florence Nyakeri) amekiuka mpaka wa uana kwa kuzuumu kuwahusisha wahusika hawa wawili kushiriki katika majukumu sawa bila kujali jinsia zao.

Katika hadithi ya *Atoke, asitoke?* Kuna mama mmoja aliyesawiriwa kuwa mlezi wa ng'ombe. Mama huyu amewasilishwa kwa kielelezo akimlisha ng'ombe nyasi (Taz. Uk.10). Jukumu la kuwasilisha mifugo kama vile ng'ombe katika jamii nyingi za Kiafrika huaminika kuwa la mwanamume (Wanjari, 2006). Kwa hiyo, kumshirikisha mhusika huyu wa kike katika utekezaji wa jukumu hili ni ukiushi wa ugavi wa majukumu kwa msingi wa uana. Vilevile, katika hadithi iyo hiyo ya *Atoke, asitoke?*, wapo kina mama wawili wanaonekana wakibeba mchanga kwa kusukuma toroli (Taz. Uk.15). Kwa mujibu wa hadithi hiyo, kina mama hawa walikuwa wakisukuma mchanga na kumwaga shimoni ili kumzika punda aliyekuwa ametumbukia humo. Hata hivyo, kinachoangaziwa ni kitendo cha mwandishi kuwatumia kina mama kusukuma mchanga kwa toroli ilhali wanaume walikuwapo. Shughuli ya kubeba mchanga kwa kusukuma kwa toroli huwa ngumu na huhitaji nguvu nyingi. Hii ni miongoni mwa shughuli za nje ya nyumbani na ambazo jamii nyingi ulimwenguni huwatengea wanaume (Mizra na Malik, 1999; Kimmel, 2004; Ahmed, 2006; McCabe na wenzake, 2011; Ullah na Skelton, 2012).

Hivyo basi, kuwashirikisha wahusika wa kike katika shughuli kama hizo kunadhihirisha ukiushi wa ugavi wa majukumu kwa misingi ya uana. Hali kama hii ndiyo inayoshuhudiwa katika hadithi ya *Vitendo vya Jamila*, ambapo mhusika mkuu ni msichana mdogo anayeitwa Jamila.

Licha ya udogo wake, Jamila anawaongoza wanafunzi wenzake kunadhifisha mazingira kijijini na shuleni. Tunamwona Jamila akichota takataka na kusukuma toroli kama inavyodhihirika kwenye jalada la kitabu cha *Vitendo vya Jamila*. Aidha, ukiushi mwingine katika hadithi hiyo, unadhihirika kupitia kielelezo cha wasichana wawili, mmoja anafyeka nyasi huku mwingine akichoma takataka (Taz. Uk.9). Shughuli ya kufyeka ni mojawapo wa majukumu ya nje ya nyumba ambayo yanahusishwa na watu wa jinsia ya kiume.

Ukiushi wa majukumu vilevile unabainika kupitia kwa mhusika Baraka katika hadithi ya *Tuzo ya Baba*. Baraka ni mvulana mdogo anayemsaidia mama yake kutekeleza majukumu ya ndani ya nyumba. Mwanzo, tunamwona akimsaidia mama yake kubeba bakuli la mboga kutoka jikoni na kulipeleka katika meza ya bwalo (Taz. Uk.10). Baada ya hapo, Baraka anamsaidia mama yake kuandika meza (Taz. Uk.12). Wanapomaliza kula, Baraka anaondoa vyombo vyote mezani na kuvipeleka jikoni. Akiwa kule jikoni, anaviosha vyombo vile (Taz. Uk.13), huku akiimba wimbo kwa furaha (Taz. Uk.14). Wimbo huo ulikuwa hivi:

“Sikiliza mama we
Nikuambie kitu we
Mikono yangu midogo
Haiwezi kufanya kazi
Nitakua mkubwa we
Nitakusaidia we
Nawe umpumzike we”
(Taz. Uk.13)

Kama ilivyobainshwa awali, majukumu ya ndani ya nyumba kama vile kuandaa vyakula, kuandika meza, kuondoa vyombo mezani baada ya kula na kuosha vyombo yananasibishwa na jinsia ya kike. Kwa hivyo, kushirikishwa kwa Baraka kutekeleza majukumu hayo kunaashiria ukiushi katika ugavi wa majukumu katika misingi ya uana.

Ukiushi mwingine wa majukumu unadhihirika pale tunapowaona wahusika wa kike wakiongoza au kuelekeza shughuli zinazoaminika katika jamii nyingi ulimwenguni kuwa za wanaume. Kwa mfano, katika hadithi *Kiki Afunga Bao*, tunakumbana na mhusika wa kike anayeitwa Bi. Atieno. Licha ya kuwa mwanamke, Bi. Atieno anatekeleza jukumu la kuwa kocha wa mchezo wa kandanda. Yeye ndiye anayeandaa timu ya kandanda shuleni. Mchezo wa kandanda aghalabu huaminika na watu wengi ulimwenguni kuwa mchezo wa kiume. Isitoshe, kocha wengi wa mchezo wa kandanda huwa wanaume. Bi. Atieno, vilevile anazuumu kumteua Kiki, ambaye ni msichana kuwa kiongozi wa timu ya kandanda shuleni, licha ya kuwapo kwa wanafunzi wavulana shuleni humo (Taz. Uk.14). Inapofika siku ya mashindano, tunagundua kuwa kocha wa timu ya shule pinzani alikuwa wa jinsia ya kiume. Hata hivyo, timu iliyoelekezwa na Bi. Atieno ndiyo iliweza kutwaa ushindi. Aidha, ukiushi wa TDU unaendelea kujitokeza zaidi kutokana na namna Kiki aliiongoza timu yake. Kiki akishirikiana na rafiki yake Mariamu (msichana), walicheza kwa bidii na ustadi mkubwa. Kiki aliwachenga wachezaji wa timu pinzani na hatimaye akafunga bao na kuipa timu yake ushindi. Msimulizi wa hadithi anatueleza hivi:

“...Kiki anauchukua mpira. Anachenga wanafunzi wengi. Anapiga mkwaju kwa mguu wake wa kulia. ‘Goal! Goal!’ Sauti zinasikika. Kiki amefunga bao. Walimu na wanafunzi wanashangilia. Uwanja mzima unajaa shangwe.” (Taz. Uk. 18)

Wahusika wengine wanaodhihirisha ukiushi sawa na huu ni Fena na Zawadi katika hadithi ya *Tuzo ya Baba* (Taz. Uk.5) na Nanjala katika hadithi ya *Kombo Arudi Shule* (Taz. Uk.15). Wahusika hawa wote ni wa kike ila wanapenda kushiriki katika mchezo wa kandanda. Mwandishi anatueleza kuwa, mhusika Fena alikuwa na ndoto ya kuchezea timu ya taifa katika mchezo wa kandanda.

“Fena alipenda kucheza mpira wa miguu. Alitamani kuchezea timu ya taifa.” (Taz. Uk. 5).

Nanjala kwa upande mwingine pia alipenda kucheza mchezo wa kandanda. Yeye pamoja na wanafunzi wenzake (wasichana wakiwemo) walipenda kucheza mchezo wa kandanda. Msimulizi anatueleza hivi:

“Nanjala na wenzake walienda uwanjani kucheza. Walipenda kucheza kandanda. Walicheza huku wengine wakishangilia. Walisubiri siku ambayo Kombo angerudi wacheze pamoja.” (Uk. 15)

Kando na kushiriki katika mchezo wa kandanda, ukiushi mwingine unajitokeza katika hadithi ya *Tuzo ya Baba* tunapomwona Baraka akishiriki katika mchezo wa kuruka kamba. Anapewa jukumu la kushika na kuruka kamba (Taz. Uk.5). Miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni hususan katika jamii za Kiafrika, mchezo wa kuruka kamba huaminika kuwa wa wasichana au wanawake. Kwa hivyo, kushirikishwa kwa mhusika mvulana (Baraka) katika mchezo huo ni ishara ya ukiushi katika ugavi wa majukumu.

Tukio lingine linaloashiria ukiushi wa TDU katika ugavi wa majukumu ni tendo la Fena katika hadithi ya *Tuzo ya Baba* kuwashurutisha Baraka na Zawadi waungane naye kupanda mti ili wachume maembe (Taz. Uk.6). Tendo la kupanda miti katika jamii za Kiafrika huaminika kuwa la wavulana au wanaume. Katika jamii nyingi za Kiafrika, hasa jamii ya Waturkana, ni mwiko kwa wanawake au wasichana kupanda miti (Ekiru, 2019). Hata hivyo, mwandishi katika hadithi hii anakata shauri kumtumia mhusika wa kike kutekeleza jukumu hilo. Hali hiyo inaashiria ukiushi wa TDU katika ugavi wa majukumu.

Mwisho, katika hadithi ya *Furaha ya Arope*, kuna tukio linalodhihirisha ukiushi wa TDU katika ugavi wa majukumu. Msimulizi anaeleza kuwa, Arope alikuwa akimsaidia mama yake kuchunga mifugo kama vile: Ng'ombe, mbuzi na ngamia (Taz. Uk.1 na 3). Kwa mujibu wa jamii ya Waturkana, jukumu la kuchunga mifugo huwa ni la wavulana au wanaume (Ekiru, 2019). Hivyo basi, kumshirikisha msichana katika jukumu hilo ni kukiuka mila na desturi za Waturkana zinazoongoza ugavi wa majukumu.

Ijapokuwa waandishi wa hadithi teule wameonyesha ukiushi wa TDU katika ugavi wa majukumu, ukiushi huu kwa kiasi kikubwa umeegemea wahusika wa jinsia ya kike. Ni wahusika wachache wa jinsia ya kiume wamekiushwa kimajukumu. Jambo hilo linaibua swali ambalo ni: Je, kwa nini waandishi wa hadithi za Kiswahili za watoto wamekiuka TDU katika ugavi wa majukumu, kwa wahusika wengi wa kike wakilinganishwa na wahusika wa kiume?

Katika kujibu swali hili, wasomi wa saikolojia ya jamii wametoa maelezo mbalimbali. Liben, Bigler na Krough (2001) wanadai kuwa huenda waandishi hususia kuwatwika wahusika wa kiume majukumu ya kike kwa sababu wanaona kuwa majukumu yanayonasibishwa na jinsia ya kike yana thamani ya chini hivyo basi kuwatwika wahusika wa kiume majukumu hayo ni sawa na kuwadunisha. Hata hivyo, waandishi wao hao wanaona wepesi kuwapa wahusika wa kike majukumu ya kiume kwa sababu kufanya hivyo ni kuwakweza na kuwasawazisha na wahusika wa kiume kihadhi.

Wasomi wengine (k.v. Thorn, 1993; DeRoser na Marcus, 2005) wanaamini kuwa, yamkini, waandishi wengi walilelewa katika mazingira ambamo TDU zilikuwa zimekithiri mno. Katika mazingira hayo, walikuzwa kuamini kuwa majukumu fulani yametengewa wanaume huku mengine yakitengewa wanawake. Hata hivyo, mazingira mengi ya kijamii huwalea watoto kuamini kuwa majukumu ya kiume huwa na dhima na hadhi kuu kuliko majukumu ya kike. Kauli hii ni sadikifu katika utafiti huu kwa kuwa waandishi 8 katika ya 11 wa hadithi hizi teule ni wa jinsia ya kiume. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa kuwa malezi na unasaba wao kijinsia uliathiri mitazamo yao katika ugavi wa majukumu.

Evans na David (2000) wakimrejelea Thorn (1993) wanadai kuwa, wavulana huelekezwa kufumbata majukumu ya kiume katika kipindi cha awali kabisa cha utotoni kuliko wasichana. Baada ya kuelekezwa, wao hujenga miundo ya uana ambayo hudhibiti mambo wanayopaswa kufanya wakiwa wanaume na yale wanayopaswa kuepuka. Hali kama ile huwatendelea pia wasichana. Thorn (keshatajwa) anasisitiza kuwa jamii hubuni miundo misingi ya kijamii inayohakikisha TDU zinazingatiwa katika jamii. Miundo misingi huwahusisha 'askari wa uana' ambao Thorn huwaita '*Gender Police*'. Askari hawa wa uana huwa ni walimu, wazazi, wafanyakazi wa shule, mahirimu, waandishi wa vitabu na watu wengine wanaopatikana katika mazingira au jamii zao. Jukumu kuu la askari wa uana huwa ni kuhakikisha watoto wamekumbatia TDU. Watoto wanaokiuka TDU huadhibiwa, hutengwa, hukaripiwa, hukejeliwa au husimangwa na askari wa uana. Wavulana wanaokiuka TDU kwa mujibu wa Evan na David (washatajwa) hupewa jina la 'Sissy' huku wasichana wakipewa jina la 'Tomboy'. Kisaikolojia, neno 'Sissy' hurejelea mwanamume mwoga, dhaifu, dhalili na asiye na nguvu ilhali 'Tomboy' humrejelea mwanamke jasiri, shujaa, bomba, mwenye nguvu na uwezo sawa na mwanamume. Yamkini, ni kwa misingi hii, waandishi hawa wanaona ni heri kumfanya mhusika wa kike kuwa 'Tomboy' kwa sababu watamkweza kihadhi kwa kumsawiri kuwa shujaa, bomba, jasiri na mwenye uwezo mkubwa kuliko kumsawiri mhusika wa kiume kama 'Sissy' kwa sababu watakuwa wanamdunisha au kumdhaliisha.

Hata hivo, Morrow (2006) anaonya kuwa mtazamo kama huu ni hatari na unapoendelezwa miongoni mwa jamii, unaweza kuwanyima wavulana fursa ya kufanya au kufurahia majukumu yanayokisiwa kuwa ya kike ijapokuwa wangependa kuyafanya. Hivyo basi, anapendekeza usawiri wa

wahusika katika vitabu vya watoto ufanywe kwa mtindo huria ili kuwawezesha watoto wa jinsia zote kushiriki katika harakati za kijamii bila kukwazwa na misingi ya uana.

Hitimisho

Makala hii imepambanua namna ukiushi wa taswira dumifu za uana katika ugavi wa kazi na majukumu kwa wahusika ulivyojitokeza kwenye hadithi teule za Kiswahili za watoto. Matokeo ya utafiti kwenye makala hii yanaonyesha kuwapo kwa mabadiliko ya kiutunzi miongoni mwa waandishi wa kisasa, ambao wamechukua mielekeo ya kiukiushi. Waandishi hawa wamejaribu kuyarekebisha mawazo ya hapo awali ambayo yaliangazia ugavi wa kazi na majukumu katika misingi ya taswira dumifu za uana. Utunzi wa hadithi za watoto katika misingi ya taswira dumifu za uana umekosolewa na wasomi wengi katika nyanja za saikolojia na fasihi ya watoto kwa sababu una athari hasi katika makuzi, maendeleo na mustakabali wa watoto.

Taswira hizi dumifu zinaweza kuathiri namna watoto wanavyojifasiri katika misingi ya uana. Taswira dumifu za uana zinaweza kuwafanya watoto kujenga imani kuwa jinsia fulani ni dhalili na dhaifu inapolinganishwa na nyingine. Taswira hizi dumifu za uana zisipodhibitiwa mapema, zinaweza kukolea na kukomaa akilini mwa watoto toka utotoni hadi ukubwani. Hali hii inaweza kusababisha kuwapo kwa kizazi kinachobaguana kwa misingi ya uana.

Kwa hivyo, juhudi kama hizi za kukabili taswira dumifu za uana kupitia utunzi wa vitabu vya watoto vilivyokiuka taswira dumifu za uana ni faafu, kwa sababu zinalenga kuvunja taasubi hasi za uana na kujenga imani kuwa, wanawake pia wanaweza kufanya kazi au majukumu yanayofanywa na wanaume. Wanaume vilevile wanaweza kufanya kazi au majukumu yanayofikiriwa kuwa ya wanawake bila kusimangwa wala kudhalilishwa. Hali hii itawapa watoto fursa ya kujenga mwelekeo mzuri wa kifalsafa kuwa ufanisi wao maishani utategemea juhudi na jitihada zao na wala si uana au jinsia zao. Mwisho, utafiti huu umedhihirisha kuwa fasihi ya Kiswahili ya watoto inakua na kubadilika kadri ulimwengu unavyobadilika.

Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, makala hii inapendekeza kuwa, vyama vya waandishi wa vitabu vya watoto vishirikiane na wizara ya elimu pamoja na wizara ya masuala ya uana na utumishi wa umma ili kubuni sera na mikakati kabambe ya namna vitabu vya watoto vinavyoweza kutumiwa kama nyenzo au vichocheo vya kuhimiza uhuru katika uteuzi wa kazi na majukumu mbalimbali katika jamii. Hali hii itasadia kuondoa vikwazo hususani vinavyowakumba wasichana au wanawake wanaoogopa kufanya baadhi ya kazi na kutelekeza majukumu fulani yanayoaminika kuwa ya wanaume. Aidha, wavulana nao hupuza au hutelekeza majukumu na kazi fulani wanayoamini kuwa ni ya wasichana au wanawake. Hii ndiyo mojawapo ya sababu kuu ya kuwapo kwa wanawake wachache katika taaluma na kazi zinazohusu sayansi asili huku wanaume wakiadimika katika taaluma za lugha, na sayansi jamii.

Kutokana na mielekeo mipya katika usawiri wa uana kwenye hadithi teule zilizotumika katika utafiti huu, makala hii inapendekeza kuwa kozi ya fasihi ya watoto ianzishwe katika vyuo vya walimu wa shule za msingi na chekechea. Ufundishaji wa fasihi ya watoto katika ngazi hizi mbili za elimu ni muhimu kwa sababu utawapa wakurufunzi maarifa kuhusu fasihi ya watoto. Utawawezesha kumaizi dhima na vipengele mbalimbali vya fasihi ya watoto katika elimu ya watoto kwenye viwango vya chekechea na shule za misingi. Utawezesha pia kutambua masuala ya uana na jinsia yanayoibuka katika vitabu vya watoto vinavyotumika shuleni, hivyo basi watakuwa na uwezo wa kuwaelekeza watoto katika uteuzi na usomaji wa vitabu vinavyokiuka taswira dumifu za uana.

Marejeleo

Agume, (2015). Upinde wa Mvua katika *Rangi Zetu* Toleo la Kwanza. Kampala: Fountain Publishers. ISBN 978-9970-25-882-6

Ahmed, N., & Hyder, K. (2006). *Gender inequality and trade liberalization: A case study of Pakistan*.

Atulo, F. (2008). *Kisa cha Mebo*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Bakize, L. (2017). Gender balance Struggles in Tanzanian Swahili children's Literature. *Kiswahili*, 79(1).

- Bem, S. L. (1981). Gender schema theory: A cognitive account of sex typing. *Psychological Review*, 88(4), 354.
- Bem, S. L. (1983). Gender schema theory and its implications for child development: Raising gender-aschematic children in a gender-schematic society. *Signs: Journal of women in culture and society*, 8(4), 598-616.
- Biem, A., Katagiri, S., & Juang, B. H. (1993, September). Discriminative feature extraction for speech recognition. In *Neural Networks for Signal Processing III-Proceedings of the 1993 IEEE-SP Workshop* (pp. 392-401). IEEE.
- Britton, G. E., & Lumpkin, M. C. (1977). For sale: Subliminal bias in textbooks. *The reading teacher*, 31(1), 40-45.
- Derman-Sparks, L., & Edwards, J. O. (2010). *Anti-bias education for young children and ourselves*. National Association for the Education of Young Children Washington, DC.
- DeRosier, M. E., & Marcus, S. R. (2005). Building friendships and combating bullying: Effectiveness of SS GRIN at one-year follow-up. *Journal of Clinical Child and Adolescent Psychology*, 34(1), 140-150.
- Derrida, J. (1976). *Of Grammatology* (tafsiri ya *De la grammtologie*). Paris: Baltimore, Md.
- Ekiru, S. E. (2019). *Exploring the use of Gender-Atypical Kiswahili children's stories to address Gender Stereotyping among Learners in a selected primary School in Trans-Nzòia County, Kenya* (Masters Dissertation, Moi University).
- Ellis, N. C. (2002). Frequency effects in language processing: A review with implications for theories of implicit and explicit language acquisition. *Studies in second language acquisition*, 24(2), 143-188.
- Esen, Y., (2007) Sexism in School Textbooks Prepared under Education Reform in Turkey'. *Journal for Critical Education Policy Studies*, 5: 109.
- Evans, L., & Davies, K. (2000). No sissy boys here: A content analysis of the representation of masculinity in elementary school reading textbooks. *Sex Roles*, 42(3-4), 255-270.
- Ezenwa-Ohaeto, E. (2015). Fighting Patriarchy in Nigerian Cultures Through Children's Literature. *Studies in Literature and Language*, 10(6), 59-66.
- Floyd, C. A. (2012). Gender Depiction in Preschool Books: A Comparison between Early Care and Education Classrooms in the United States and Norway. *Electronic Theses and Dissertations*. 203. Available at <https://digitalcommons.du.edu/etd/203>
- Fox, M. (1993) 'Men Who Weep, Boys Who Dance: The Gender Agenda Between the Lines in Children's Literature in Language Arts pp. 84-88.
- Golshirazian, S., Dhillon, M., Maltz, S., Payne, K. E., & Rabow, J. (2015). The Effect of Peer Groups on Gender Identity and Expression. *International Journal*, 9.
- Islam, K. (2008). *Sungura Mjanja Mjanja*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kalindimya, J. (2008). *Khadija na Baiskeli Nyekundu*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Lewela, M. (2008). *Kombo Arudi Shule*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Liben, L. S., & Signorella, M. L. (1980). Gender-related schemata and constructive memory in children. *Child Development*, 11-18.
- Liben, L. S., Bigler, R. S., & Krogh, H. R. (2001). Pink and blue collar jobs: Children's judgments of job status and job aspirations in relation to sex of worker. *Journal of Experimental Child Psychology*, 79(4), 346-363.
- Martin, C. L., & Halverson Jr, C. F. (1981). A schematic processing model of sex typing and stereotyping in children. *Child Development*, 1119-1134.
- Matundura, E. S. (2007). *Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto* (Masters dissertation, University of Nairobi).
- Mbuthia, D. E. M. (2018). The Role of Kiswahili Children's Literature in formulating their World view. *International Journal of Educational Research*. Vol.6 (2)129-140

- McCabe, J., Fairchild, E., Grauerholz, L., Pescosolido, B. A., & Tope, D. (2011). Gender in twentieth-century children's books: Patterns of disparity in titles and central characters. *Gender & Society*, 25(2), 197–226.
- Meland, A. T. (2020). Challenging gender stereotypes through a transformation of a fairy tale. *European Early Childhood Education Research Journal*, 28(6), 911-922.
- Miller, N. (2013). *Reimagining Shakespeare for children and young adults*. Routledge.
- Miricho, E. M. (2021). Ukiushi wa Kanoni katika Hadithi Teule za Watoto za John Kobia na Wadi Wamitila. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Miricho, M., & Mbutia, E. M. (2017). *The impact of the depiction of children in selected Swahili children stories*.
- Mirza, M. and R. Malik, (1999). Gender Analysis of Primary School Textbooks in Punjab'. Lahore: Department of Women's Studies (unpublished report).
- Mogambi, H. (2006). *Vitendo vya Jamila*. Nairobi. Moran Publishers.
- Morrow, V. (2006). Understanding gender differences in context: implications for young children's everyday lives. *Children & society*, 20(2), 92-104.
- Mosley, J. (2004). Gender and daily life in Ethiopia. *Contemporary Review*, 97-101.
- Mwangi, W. (2009). *Atoke Asitoke?* Nairobi: Oxford University Press.
- Nhundu, T. J. (2007). Mitigating gender-typed occupational preferences of Zimbabwean primary school children: The use of biographical sketches and portrayals of female role models. *Sex Roles*, 56(9–10), 639–649.
- Nhundu, T. J. (2007). Mitigating gender-typed occupational preferences of Zimbabwean primary school children: The use of biographical sketches and portrayals of female role models. *Sex Roles*, 56(9–10), 639–649.
- Nyakeri, F. (2006). *Siku za Juma 1a*. Nairobi: Oxford University Press.
- Onyango, J. O. (2007). Masculinities in Kiswahili Children's Literature in Kenya (Vol. 14, pp. 245–254). Presented at the Swahili Forum.
- Onyango, O. (2006). Dark Shadow of Masculinities and Women Emancipation Agenda. *CODESRIA Bulletin Special Issue on the African Woman*, 36–38.
- Preece, S., & Bullingham, R. (2022). Gender stereotypes: The impact upon perceived roles and practice of in-service teachers in physical education. *Sport, Education and Society*, 27(3), 259-271.
- Rorty, R. (1996). Pragmatism and law: A response to David Luban. *Cardozo L. Rev.*, 18, 75.
- Rukaria, M. (2008). *Kiki Afunga Bao*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Ullah, H. (2013). The Reproduction of Class and Gender Hierarchies through Different Education System in Khyber PakhtunKhwa. Ph.D Dissertation, University of Peshawar, Pakistan.
- Ullah, H., & Skelton, C. (2012). Gender Representation in the Public Sector Schools Textbooks of Pakistan. *Educational Studies*. 1 (12), 1–12. doi:10.1080/03055698.2012.702892. [Taylor & Francis Online]
- Ullah, H., Ali, J., & Naz, A. (2014). Gender representation in children's books: A critical review of empirical studies. *World Applied Sciences Journal*, 29(1), 134-141.
- Wafula, R. & Njogu, K. (2007). *Uhaki wa Fasihi na Nadharia*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundations.
- Walibora, K. (2013). *Furaha ya Arope*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wanjeri, M. M. (2006). *Language and gender: Male domination among the Kikuyu of Kenya*, East Africa. Available at: https://www.researchgate.net/publication/306025311The_cultureofgrowingup/citation/download
- Zawadi, R. (2013). *Tuzo ya Baba*. Nairobi: Queenex Publisher Limited.